



AZIMIO NA. 1/2016

AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA UDHIBITI WA MATUMIZI YA DAWA NA MBINU ZA KUONGEZA NGUVU MICHEZONI (*INTERNATIONAL CONVENTION AGAINST DOPING IN SPORT*)

KWA KUWA, Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni yaani UNESCO;

NA KWA KUWA, Mkutano Mkuu wa UNESCO, katika kikao cha 33, kilichofanyika Paris kuanzia tarehe 3 – 21 Oktoba, 2005 uliridhia kuandaliwa Mkataba wa Kimataifa wa Udhhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu katika Michezo;

NA KWA KUWA, Tanzania ilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mkutano (*General Committee*) iliyoshiriki katika majadiliano yaliyowezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Udhhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu katika Michezo;

NA KWA KUWA, Mwaka 2003 Mjini Paris, katika Kikao cha Mawaziri wenye dhamana ya Elimu ya Michezo kutoka nchi 103 wanachama wa UNESCO walipendekeza kuanzisha Chombo cha Kisheria kitakachotambulika Kimataifa kwa ajili ya udhibiti wa matumizi ya Dawa na Mbinu haramu katika michezo;

NA KWA KUWA, Malengo ya UNESCO ni kuhimiza Amani na Usalama kwa kuendeleza mahusiano baina ya Mataifa kupitia Elimu, Sayansi na Utamaduni;

NA KWA KUWA, Michezo inasaidia kuchochea Amani, kulinda Afya na kujenga mahusiano Kimataifa;

NA KWA KUWA, Matumizi ya Dawa na Mbinu haramu katika Michezo yanaleta matokeo ambayo sio ya haki na sawa katika michezo na athari mbalimbali za kisaikolojia na kiafya kwa wachezaji na hasa vijana;

NA KWA KUWA, Hapa nchini tatizo la matumizi ya Dawa na Mbinu haramu katika michezo limeanza kujitokeza katika baadhi ya michezo;

NA KWA KUWA, Mkataba huu unalenga kuimarisha mapambano dhidi ya Matumizi ya Dawa na Mbinu zilizopigwa marufuku katika michezo;

NA KWA KUWA, Ibara 36 ya Mkataba huu inazitaka Nchi wanachama kuridhia na kuwasilisha Hati ya Kuridhia kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO;

NA KWA KUWA, Hadi sasa katika Bara la Afrika nchi 7 ndizo ambazo hazijaridhia Mkataba huo na katika nchi za Afrika Mashariki ni Tanzania pekee ambayo bado haijaridhia;

NA KWA KUWA, Tanzania kwa kuridhia Mkataba huu na hatimaye kuutekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:-

- (a) Kuwajengea wanamichezo utamaduni wa kushindana kwa haki na ari ya kujituma kwa kutegemea uwezo wao wenyewe;
- (b) Kulinda na kuimarisha afya ya wanamichezo wetu;
- (c) Kujijengea imani na heshima kwa mataifa mengine;
- (d) Kuwezesha Tanzania kuhudhuria mafunzo, mikutano na vikao vya Kimataifa na kushiriki katika makongamano na hata kuwa mwenyeji wa makongamano yenye maamuzi mbalimbali yanayohusu suala hili;

- (e) Kuwa na fursa ya kuchagua ama kuchaguliwa kuongoza vyombo vya kimataifa vinavyoundwa chini ya Mkataba;
- (f) Kupata misaada ya wataalamu, fedha, vifaa na mafunzo kwa ajili ya utekelezaji wa makubaliano haya;
- (g) Kufanya tafiti au kutumia matokeo ya tafiti ya Wadau wengine katika kudhibiti matumizi ya dawa na mbinu za kuongeza nguvu katika michezo, na
- (h) Kuwezesha Tanzania kushiriki na kuandaa mashindano mbalimbali ya kimataifa.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Tatu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu katika Michezo yaani (*International Convention Against Doping In Sport*).

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 6 Juni, 2016

Dkt. Thomas D. Kasilillah
KATIBU WA BUNGE